Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative

Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini Mafuta na Gesi Asilia

# TAARIFA SEMINA YA KUELIMISHA VIONGOZI WA WENYE ULEMAVU HAFIFU KUTOKA KATIKA WILAYA ZA MKOA WA DODOMA




**DODOMA**

**FEBRUARI 22, 2025**

## 1. UTANGULIZI

Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI), ilifanikiwa kufanya Semin katika Mkoa wa Dodoma tarehe 22 Februari, 2025. Semina hiyo ilifunguliwa na Mgeni rasmi CPA Ludovick Utouh, mwenyekiti wa Kamati ya TEITI na kuhudhuriwa na viongozi, wenyeviti, wajumbe, weka hazina mbalimbali kutoka katika wilaya za mkoa wa Dodoma, Chamwino, Bahi, Chemba, Kondoa, Dodoma mji, Kongwa, Mpwapwa, UDOm, Shule ya msingi Buigiri, Shule ya msingi Homboro.

Semina hii ililenga kuelimisha wananchi wenye uoni hafifu juu ya matumizi ya taarifa zilizopo kwenye ripoti ambazo hutolewa na Taasisi ya TEITI ambayo huweka wazi taarifa za leseni zilizotolewa kwa kipindi husika, taarifa za malipo ya ushuru wa huduma (*Service Levy*), ushirikishwaji wa wananchi katika utoaji huduma za bidhaa *(Local Content),* pamoja na ajira na uwajibikaji wa makampuni ya uziduaji kwa jamii (CSR).

Aidha, TEITI imekuwa ikitekeleza majukumu yake na kuhakikisha Kampuni zinazofanya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia hapa nchini zinaweka wazi taarifa za shughuli zao kulingana na viwango vya Taasisi ya Kimataifa ya Uhamasishaji wa Uwazi Katika Sekta ya Uziduaji (*EITI*) na Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania ya Mwaka 2015 (Sheria ya TEITA ya Mwaka 2015). Jukumu lingine la TEITI ni kuwajengea uwezo wananchi katika kutumia taarifa na takwimu zinazotokana na shughuli za uendeshaji wa makampuni ya uziduaji hapa nchini, kwa ajili ya kuhoji Serikali kuhusu mapato yanayopatikana kwenye Sekta ya Uziduaji na hivyo kuhamasisha mijadala kuhusu manufaa ya uchimbaji madini, mafuta na gesi asilia hapa nchini.

Mwakilishi wa mgeni rasmi Bw. Erick Ketagory wakati akifungua Semina hii, alilisitiza kuwa uziduaji wahakikishe kwamba wanaweka wazi taarifa na takwimu za uzalishaji na mauzo ya bidhaa zao na kuajiri wananchi pamoja na kutumia bidhaa na huduma zipatikanazo ndani ya nchi.

## 2. Mpango wa Kuelimisha Umma, Serikali na Asasi za Kiraia

Katika kutekeleza shughuli za TEITI kwa lengo la kuboresha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia chini TEITI iliona fursa kutoa semina kwa wananchi wenye uoni hafifu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake pia kwa ajili ya kuhamasisha matumizi ya taarifa na takwimu zinazotolewa katika ripoti za TEITI za kila mwaka. Semina hii ni utekelezaji wa shughuli zinazolenga kufanya uhamasishaji huu ni Mkoa wa Dodom mji.

Lengo ya Semina hii ni pamoja na kuhamasisha kuhusu matumizi ya taarifa na takwimu zinazotolewa katika ripoti za TEITI kwa wanachama, wananchi wenye uoni hafifu kutoka katika wilaya saba (7) za mkoa wa Dodoma. Aidha, semina hii pia ililenga kuitangaza Taasisi ya TEITI pamoja na majukumu yake kwa washiriki.




**Picha Na.1**: Mwakilishi wa mgeni rasmi ambae pia ni Kaimu Mkuu wa KItengo cha Uwazi na Uwajibikaji Bw. Erick Ketagory *akiwasilisha hotuba ya ufunguzi wa Warsha tarehe 20 Februari, 2025.*

**Picha Na.2**: *Mwaklishi wa Katibu Mtendaji wa TEITI ambae pia ni Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Tehama na Takwimu Bw. Bakari Birika akitoa neno wakati wa ufunguzi wa Semina wa watu wenye uoni hafifu.*

Ni dhamira ya Serikali kuendesha shughuli zake kwa uwazi na kuhakikisha kuwa wananchi wanashiriki kikamilifu katika usimamizi wa uvunaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia. Hivyo, ni muhimu kuwajengea uwezo wananchi kuhusu namna ya kuchambua taarifa na takwimu zilizopo katika ripoti za TEITI pamoja na kuzitumia katika kuhoji na kuibua mijadala itakayosaidia kuboresha Sekta ya Uziduaji hapa nchini.

## 3. Washiriki katika Semina

Semina hii ilifunguliwa na mwakilishi wa mgeni rasmi Bw. Erick Ketagory. Ufunguzi huu ulitanguliwa kwa kuisoma hotuba ya Mwenyekiti wa TEITI, CPA. Ludovick S. Utouh. Washiriki mbalimbali walihudhuria warsha hii. Aidha, wageni wengine walioshiriki ni pamoja na waandishi wa habari. Ketagory alisema pia TEITI imekuwa ikiandaa na kuchapisha kwa waandishi maalum ya nukta nundu ili kuwafikia kundi la wananchi wasioona hapa nchini, mtakumbuka kuwa rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asili ni za wananchi wote.

“Hivyo TEITI imeona ni vyema kuandaa ripoti zetu kwa nukta nundu ili wananchi wote wapate fursa ya kuelewa na kufahamu juu ya taarifa na takwimu mbalimbali katika sekta Madini, Mafuta na Gesi Asilia ili waweze kuhoji manufaa ya rasilimali hizo kwa nchi na wananchi.”

Akisoma hotuba ya Katibu Mtendaji wa TEITI, Mariam Mgaya, Kaimu mkuu wa kitengo cha Tehama na Takwimu TEITI, Bakari Birika katika warsha hiyo washiriki watapata fursa ya kupata uelewa kuhusu majukumu ya TEITI na namna ya kutumia takwimu zinazoandaliwa kupitia Ripoti za TEITI.

“Taasisi inajukumu la kujenga mfumo wa uaandaji wa Ripoti za TEITI na kuwajengea uwezo wananchi katika kutumia Takwimu zinazotokana na taarifa za TEITI kupitia warsha mbalimbali na ndio maana tumeandaa semina hii kwa kundi hili ili nao wawe na mchango wa kuchangia katika sekta hizi.”

**Picha washiriki kutoka katika Wilaya mbalimbali za mkoa wa Dodoma**







Mgeni Rasmi:- CPA. LUDOVICK UTOUH
MWENYEKITI WA KAMATI YA TEITI
20 FEB
DODOMA
TEITI

•


WARSHA MAALUM YA KUWAELIMISHA
WANANCHI WASIOONA KUHUSU MATUMIZI
YA TAKWIMU ZINAZOTOLEWA NA RIPOTI ZA TEITI.
Mgeni Rasmi:- CPA. LUDOVICK
TEITI


YA TAKWIMU ZINAZOTOLEWA NA RIPOTI
Mgeni Rasmi:- CPA. LUDOVICK UTOUH
DODOMA
TEITI

**Picha Na. 4**: *Wakirishi kutoka Wilaya mbalimbali za mkoa wa Dodoma.*

## 4. Mada zilizowasilishwa katika Warsha

Mada mbalimbali ziliwasilishwa katika semina hii ili kuweza kuwafikishia ujumbe walengwa na kufikia malengo ya warsha hii kwa kuwatumia watoa mada wafuatao:- Mtoa mada Bw. Erick Ketagory, Afisa kutoka TEITI alitoa mada kuhusu, *"Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania (TEITI)"*, *"Majukumu ya Asasi za Kiraia katika Utekelezaji wa Shughuli za Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia"* na, *"Uwajibikaji wa Makampuni kwa Jamii (Corporate Social Responsibility (CSR) na Ushiriki wa Wananchi katika kutoa Huduma na Bidhaa (Local Content) katika Sekta ya Uziduaji".*

### 4.1 Utekelezaji wa Kazi na Majukumu ya Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania.

Mada hizi ziliwasilishwa kwa lengo la kuelimisha washiriki kuhusu Taasisi ya TEITI pamoja na majukumu yake ili kuongeza uelewa wa Taasisi hiyo. Aidha, mtoa mada alisisitiza zaidi katika kuhamasisha matumizi ya taarifa na takwimu zinazotolewa katika ripoti za TEITI ili kusaidia umma kupata uelewa wa kila taarifa na takwimu hizo.

**Picha Na.5**: *Bw. Erick Ketagory, Afisa kutoka TEITI akitoa mada kuhusu Majukumu ya Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania.*

## 5. Changamoto na Mapendekezo

Semina hii imetoa picha kuwa wananchi wengi wanauelewa mdogo katika matumizi ya taarifa na takwimu zinazotolewa kwenye ripoti za TEITI za kila mwaka. Aidha, Halmashauri nyingi haziwajibiki kufuatilia mapato yake ya tozo ya ushuru wa huduma kutoka katika makampuni ya uziduaji. Sambamba na hili, semina hii imekuwa sehemu ya kuweka wazi na kuibua fursa kwa wananchi wenye ulemavu wa macho mkoa wa Dodoma.

## 6. Tathmini ya Mafanikio ya Semina

i. Semina hii imetoa mwanga kuhusu uelewa wa washiriki namna bora TEITI inavyofanya shughuli za uziduaji, hatua ambayo inasaidia kuongeza uwazi na uwajibikaji.

## 7. Gharama za Warsha

Jumla ya **Tsh 13,035,000.00** zimetumika katika kufanikisha warsha hii.

## 8. Hitimisho

Taasisi ya TEITI inaendelea kuishukuru chama cha wasioona TLD na Shivywata kwa kuitikia wito na kujumuika katika semina hii kwa wananchi kutoka katika wilaya za mkoa wa Dodoma. Aidha, TEITI itaendelea kuhamasisha kuhusu umuhimu wa kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika kampuni za uziduaji ili kuwe na mafanikio makubwa zaidi katika uchangiaji wa uchumi wa nchi kutoka Sekta ya Uziduaji.

**Kiambatisho Na.1**: Barua - Kibali kwenda chama cha Shivywata

**Kiambatisho Na. 2:** Majina ya Washiriki wa Warsha.

.

***Kiambatisho Na. 3:*** *Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya TEITI CPA. Ludovick S.Utouh.*